## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## TAARIFA KWA UMMA KUHUSU NYARAKA ZA MAZINGIRA NA KIJAMII ZA MRADI WA KUKUZA USIMAMIZI ENDELEVU WA UVUVI NA UKUZAJI WA VIUMBE MAJI WA BAHARI TANZANIA (TASFAM - P179969)

**SERIKALI** ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Tanzania Bara), Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi (Zanzibar) na Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu imeandaa Mradi wa Kukuza Usimamizi Endelevu wa Uvuvi na Ukuzaji wa Viumbe Maji wa Bahari Tanzania kwa ufadhili wa Benki ya Dunia. Mradi unatarajiwa kuanza katika Mwaka wa Fedha 2025/2026. Lengo la mradi wa TASFAM ni kuimarisha usimamizi wa rasilimali za bahari na kuboresha upatikanaji wa fursa za kiuchumi kwa walengwa.

Mradi wa TASFAM unatarajiwa kutekelezwa katika maeneo ya mwambao wa Bahari ya Hindi, ukihusisha Wilaya 17 za Tanzania Bara, Wilaya 11 za Zanzibar na ukanda maalum wa kiuchumi wa Bahari ya Hindi. Walengwa wa mradi huu ni jamii za mwambao zinazojihusisha na minyororo ya thamani ya uvuvi na ukuzaji viumbe maji bahari.

Ili kudhibiti madhara katika mazingira na kijamii yanayoweza kutokana na utekelezaji wa shughuli za mradi, nyaraka zifuatazo zimeandaliwa: (i) Mpango wa Uwajibikaji wa Mazingira na Kijamii (ESCP); (ii) Mpango wa Ushirikishwaji Wadau (SEP) ikijumuisha Mfumo wa Malalamiko (GRM); (iii) Taratibu za Usimamizi wa Ajira (LMP); (iv) Mfumo wa Usimamizi wa Mazingira na Kijamii (ESMF) na Machakato wa Kushirikisha Jamii katika Maeneo ya Hifadhi (PF). Nyaraka zimeandaliwa kukidhi sera za mazingira na kijamii za kitaifa na Benki ya Dunia. Nyaraka hizi zinapatikana katika tovuti zifuatazo: https://.mifugouvuvi.go.tz/TASFAM/; https://blueeconomysmz.go.tz/TASFAM; na https://www.dsfa.go.tz/TASFAM.

Hivyo, Serikali inakaribisha wadau na umma kutoa maoni kuhusu nyaraka husika kupitia anuani zifuatazo:-


Katibu Mkuu,
Wizara ya Mifugo na Uvuvi,
Mji wa Serikali - Mtumba,
Mtaa wa Michezo,
S.L.P 2847,
**40487 DODOMA.**
Simu: 255 (026) 2322612
Nukushi: 255 026) 2322613
Barua Pepe: barua@mlf.go.tz

Katibu Mkuu,
Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi,
S.L.P 149,
Jengo la Zura, Maisara,
70468 Mjini Magharibi,
ZANZIBAR.
Simu : +255 24 2941195 /
+255 24 2941197
Barua Pepe: info@blueeconomysmz.go.tz

Mkurugenzi Mkuu,
Mamlaka ya Usimamizi wa Uvuvi wa Bahari Kuu,
S.L.P 56, Fumba,
**ZANZIBAR**
Simu: +255779888241/
+255779888215
Barua Pepe: barua@dsfa.go.tz